KISWAHILI - CBC GRADE 4 END OF TERM 2 EXAMS 2023

MASWALI

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 1-5
(Ni wakati wa likizo fupi.Hamisi na Zainabu wanakutana)
Hamisi: U hali gani Zainabu? Kumbe nawe waishi huku Tushauriane kama mimi!
Zainabu: Hali yangu ni njema. Naam. Tulihamia huku Tushauriane kwa kuwa mwenye nyumba alitaka kuipaka rangi nyumba yote.
Hamisi: Kabla ya kufunga shule hukuwa umeniambia kuwa umekuwa jirani yangu(wote wanacheka) Yaani tunasoma katika darasa moja na huwezi kuni...
Zainabu: Aaah! Nawe! Samahani basi. Huenda nilisahau. Hata hivyo, tutarudi Mnarani ufundi ukikamilika.
Hamisi: Sawa kabisa. (akikohoa kidogo)Nilikuwa nikielekea kwa kina Fauzia anieleze namna ya kutumia viunganishi katika
Zainabu: Usihofu Hamisi. Tukakae pale kivulini nikusaidie. (wakielekea chini ya mti) Je, unajua mifano gani ya viunganishi?
Hamisi: Lakini, kwa sababu, ingawa, ila na vingine vichache. Tatizo langu ni kuvitumia katika sentensi
Zainabu: Haya tukae nikuonyeshe. (wanaketi huku Hamisi akitoa daftari, kitabu na kalamu mkobani.)

1. Kulingana na mazungumzo haya,kina Zainabu walikuwa wakiishi wapi kitambo?
    A. Tushauriane.
    B. Mnarani.
    C. Kivulini.
    D. Hatujaelezwa.
2. Je, ni kwa nini familia ya Zainabu ilihama?
    A. Wazazi walitaka waishi karibu na shule
    B. Zainabu alitakiwa kuwa karibu na Hamisi ili amsaidie kimasomo.
    C. Nyumba ya kina Zainabu ya kitambo ilikuwa ikipakwa rangi.
    D. Waliupenda mtaa wa Tushauriane.
3. Unadhani Hamisi alifika kwa kina Fauzia?
    A. La.
    B. Naam.
    C. Haiwezekani.
    D. Yawezekana.
4. Tatizo la Hamisi lilikuwa gani?
    A. Kujua mifano ya viunganishi.
    B. Alitaka Zainabu amwambie kuwa walikuwa wamehama. shule.
    C. Kutaka kuhamia Mnarani.
    D. Hakujua kutumia viunganishi katika sentensi.
5. Inawezekana kuwa Fauzia ni